Imetolewa tarehe: 13 Agosti, 2010

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU KUWEPO KATIKA SOKO VYAKULA AMBAVYO NI BANDIA AU AMBAVYO HAVIJASAJILIWA

1. Utangulizi

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yenye jukumu la kudhibiti ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ili kulinda afya za watumiaji.

TFDA inapenda kuutaarifu umma kuwa, katika kaguzi zake mbalimbali katika Mkoa wa Dar es Salaam na hasa maeneo ya kuuzia vyakula, imebaini uwepo wa bidhaa bandia na ambazo hazijasajiliwa na Mamlaka na hivyo usalama na ubora wake kutothibitishwa. Bidhaa zilizokamatwa ni makopo ya maziwa ya watoto wachanga kiasi cha kopo 2,261. Mamlaka imebaini uwepo wa maziwa bandia aina ya NAN 2 yenye alama za utambuzi kama ambavyo imeainishwa hapa chini;

Aina ya Bidhaa	Ujazo	Alama za utambuzi wa maziwa halisi	Alama ya utambuzi wa maziwa bandia
NAN 2 (kopo 26)	400g	Mtengenezaji: Nestl'e France, SAS, F-77446, Mame la Vallee, Cedex 2, France Lugha: Imeandikwa kwa lugha ya kiingereza na kiswahili Lebo: Kuna picha moja ya ndege watatu weupe ambayo ni sehemu ya nembo ya Kampuni ya Nestle	Mtengenezaji: Nestl'e (South Africa (Pty) Ltd, 192 Hendrik Verwoerd Drive, Randburg, 2194, South Africa. Lugha: Imeandikwa kwa lugha mbili yaani kiingereza na lugha nyingine isiyofahamika. Lebo: Ina picha mbili za ndege watatu weupe ambapo ndege mkubwa akiwalisha ndege wawili wadogo kwenye kiota. Tarehe ya kutengenezwa: 7/09/2010 Tarehe ya kuisha matumizi: 7/3/2011 Namba ya Bachi: 82510179B2 Maziwa: Yanatoa harufu mbaya ya kuharibika.

Aina ya Bidhaa	Ujazo	Alama za utambuzi wa maziwa halisi	Alama ya utambuzi wa maziwa bandia
		Maandishi yamechapishwa kwenye kopo moja kwa moja.	Maandishi yamechapishwa kwenye karatasi na kubandikwa.

Pamoja na kukamata maziwa ya watoto yasiyokidhi viwango, Mamlaka pia imebaini kuwepo baadhi ya bidhaa nyingine za vyakula zisizokidhi matakwa ya Sheria, hizi pamoja na tomato na chilli sauce kiasi cha chupa 93 na makasha ya pipi na biskuti kiasi cha pakiti 149. Alama za utambuzi za bidhaa hizo ni kama ifuatavyo:

(i) Eyakho Chilli Sauce ambayo imefungashwa kwenye chupa angavu ya lita 2, chilli sauce ina rangi nyekundu isiyokolea, kifuniko chenye rangi ya kijani, lebo inabanduka kirahisi, anuani iliyoandikwa ni 5 Henry Nxumalo Street, Newton, JHB (0767721490) na tarehe za kusindika na mwisho wa matumizi hazijaoneshwa.

(ii) Al's Sauces Tomato Sauce, imefungashwa kwenye chupa ya ujazo wa lita 2, haina anuani ya mtengenezaji, sauce ina rangi nyekundu iliyokolea, kizibo chenye rangi nyeupe, haina tarehe ya kusindika na mwisho wa matumizi. Imeandikwa anuani ya 17 Buchan Street, Strattford Park, Turffontein.

(iii) Al's Sauces Chilli Sauce imefungashwa kwenye chupa nyekundu isiyoangavu yenye ujazo wa Ml. 500 na haina tarehe ya kusindika na mwisho wa matumizi.

Vilevile Mamlaka imebaini uwepo wa bidhaa za biskuti na pipi ambazo zimeandikwa kwa lugha ambazo si Kiswahili wala Kiingereza kinyume na Sheria na baadhi zikiwa zimekwisha muda wa matumizi.

2. Hatua zilizochukuliwa

2.1 Mamlaka inasitisha kwa muda uingizaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya maziwa aina ya NAN 2 hadi hapo uchunguzi utakapokamilika na taarifa kutolewa na Mamlaka.

2.2 Bidhaa zote zilizokutwa na upungufu uliotajwa hapo juu, zimekamatwa na kuzuiliwa kuuzwa. Aidha kaguzi bado zinaendelea ili kubaini maeneo mengine ambayo bado yanauza bidhaa hizo.

2.3 Sampuli za maziwa ya watoto wachanga ya NAN 2 zimewasilishwa maabara ili kupata taarifa zaidi kuhusu usalama wa maziwa hayo.

2.4 Mamlaka iko kwenye hatua za mwisho za uchunguzi ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.

2.5 Taarifa imeshatolewa katika Ofisi za TFDA za Kanda pamoja na ofisi za Afya za Mikoa na Halmashauri ili ufuatiliaji wa karibu wa bidhaa hizo ufanyike nchi nzima.

3. Rai kwa umma

3.1 Mamlaka inawashauri wananchi kutumia maziwa ya watoto wachanga ambayo yamesajiliwa. Maziwa hayo ni Lactogen 1 Infant Formular, Lactogen 2 Follow up Formular, na Cowbell Infant Formular yote yanatengenezwa na kampuni ya Ufaransa na NAN 1 Starter Infant Formular yanayotengenezwa Uholanzi.

3.2 Kuwa makini wakati wa kununua bidhaa hizo na zingine kwa ujumla hususan katika maelezo ya kwenye lebo ili kuweza kubaini bidhaa ambazo hazikidhi viwango.

3.3 Kutoa taarifa haraka iwezekanavyo pale watakapohisi kuuzwa kwa bidhaa hizo. Taarifa zitolewe katika ofisi ya TFDA zilizoko Barabara ya Mandela, EPI Mabibo External, Dar es Salaam na Ofisi za Kanda za TFDA zilizopo Mtaa wa Nkurumah-Mwanza, Mtaa wa Sakina – Arusha na jengo la ofisi ya Mifugo – Mbeya pamoja na ofisi za Afya za Mikoa na Halmashauri.

3.4 Wamiliki wa maduka ya chakula wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanauza vyakula vilivyosajiliwa na Mamlaka na kutoa taarifa kuhusu watu au wafanyabiashara wanaojihusisha na uuzaji wa bidhaa watakazozitilia mashaka. Aidha, wote wenye maziwa ya NAN 2 wanapaswa kuzisalimisha ofisi za TFDA na ofisi za Afya za Mikoa na Halmashauri.

4. Hitimisho

4.1 Mamlaka inapenda kusisitiza kuwa yeyote atakayepatikana akijihusisha na uuzaji wa bidhaa hizo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

4.2 Mamlaka inatoa shukrani za dhati kwa wananchi pamoja na vyombo vya habari ambao wamekuwa wakitoa taarifa zinazofanikisha kupatikana kwa bidhaa hizi zisizokidhi ubora na usalama.

Limetolewa na:

Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA),
Barabara ya Mandela, Mabibo-External,
S.L.P 77150, Dar es Salaam.

Simu: +255 222 450512/450751/452108
Nukushi: +255 222 450793
Barua Pepe: info@tfda.or.tz; Tovuti: www.tfda.or.tz

1

Ofisi za Kanda:

TFDA – Kanda ya Ziwa,
Mtaa wa Nkurumah,
S.L.P. 543,
Mwanza.
Simu: +255 28 2500733
Nukushi: +255 28 2541484
Barua Pepe: mwanza@tfda.or.tz ,

TFDA – Kanda ya Kaskazini,
Eneo la Sakina
S.L.P. 16609
Arusha.
Simu: +255 27 2547097
Nukushi: +255 27 2547098
Barua Pepe: arusha@tfda.or.tz

TFDA – Nyanda za Juu Kusini,
Jengo la Mkoa la Mifugo, S.L.P. 6171, Mbeya.
Nukushi: +255 25 2504425
Simu:+255 25 2504425
Barua Pepe: mbeya@tfda.or.tz -

TFDA – Kanda ya Mashariki,
Jengo la Makao Makuu ya TFDA,
Barabara ya Mandela, Mabibo
External, S.L.P. 77150
Dar es Salaam.
Simu: +255 22 2450512/2450751/
2452108
Nukushi: +255 22 2450793
Barua Pepe: info@tfda.ot.tz